**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TAKWIMU ZA PATO LA TAIFA ZILIZOREKEBISHWA MWAKA WA KIZIO 2015, TANZANIA BARA

## MUHTASARI WA TAARIFA

**OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU**
**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

**DODOMA**

**Februari, 2019**

**Yaliyomo**

1.0 UTANGULIZI .......... 2
1.1 Chimbuko .......... 2
1.2 Umuhimu wa Marekebisho ya Pato la Taifa .......... 3
1.3 Vyanzo vya Taarifa za Marekebisho ya Takwimu za Pato la Taifa .......... 3
1.4 Mbinu Zilizotumika Kutayarisha Pato la Taifa kwa Mwaka Kizio 2015 .. 4
1.5 Upatikanaji wa Takwimu za Pato la Taifa Zilizorekebishwa .......... 4
2.0 TAKWIMU ZA PATO LA TAIFA ZILIZOREKEBISHWA .......... 4
3.0 MATUMIZI YA TAKWIMU ZA PATO LA TAIFA .......... 5
4.0 MUHTASARI WA MATOKEO YA MAREKEBISHO .......... 6
4.1 Matokeo Muhimu .......... 6
4.2 Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa .......... 6
4.3 Viwango vya Ukuaji na Mchango wa Ukuaji katika Uchumi .......... 7
4.4 Pato la Wastani la Mwananchi .......... 8
4.5 Viwango vya Ukuaji, Takwimu za Pato la Taifa kwa Robo Mwaka .......... 8
6.0 VIAMBATISHI .......... 9

# TAKWIMU ZA PATO LA TAIFA ZILIZOREKEBISHWA KWA MWAKA WA KIZIO WA 2015 TANZANIA BARA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Chimbuko

Historia ya kutayarisha takwimu za Pato la Taifa Tanzania Bara ilianza mwaka 1954. Tangu kipindi hicho, yamefanyika maboresho katika wigo wa shughuli zote za kiuchumi kwa kuzingatia miongozo ya kimataifa. Takwimu za Pato la Taifa za vipindi vilivyopita zimekuwa zikitayarishwa kwa kuzingatia dhana, tafsiri na miongozo ya kuanisha shughuli za kiuchumi katika mifumo ya ukokotoaji wa takwimu za Pato la Taifa *(Systems of National Accounts – SNAs)* ya mwaka 1953, 1968 na 1993.

Hadi sasa, yamefanyika marekebisho katika awamu sita ya takwimu za Pato la Taifa kuanzia mwaka 1954. Marekebisho ya kwanza yalitumia kizio cha mwaka 1966 na yalizingatia Mfumo wa Mwaka 1953, marekebisho ya pili yalitumia kizio cha mwaka 1976 na yalizingatia Mfumo wa Mwaka 1968, marekebisho ya tatu yalitumia kizio cha mwaka 1992 na yalizingatia Mfumo wa Mwaka 1968 na kwa sehemu ya Mfumo wa Mwaka 1993. Aidha, marekebisho ya nne yalitumia kizio cha mwaka 2001 na yalizingatia Mfumo wa Mwaka 1993. Marekebisho ya tano yalitumia mwaka wa kizio 2007 na yalizingatia Mfumo wa Mwaka 1993 na sehemu ya Mfumo wa Mwaka 2008. Marekebisho ya sita yametumia kizio cha mwaka 2015 na yamezingatia Mfumo wa Mwaka 2008.

Marekebisho ya takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka wa kizio 2015 yametumia Mizania ya Ugavi na Matumizi *(Supply and Use Tables)* kazi hii ilianza Septemba 2017 ikihusisha watalaam wa Idara ya Pato la Taifa na ushauri wa kiufundi kutoka kwa Mshauri Mwelekezi na watalaam wa Shirika la Fedha Duniani (IMF).

Lengo la marekebisho yaliyotumia kizio cha mwaka 2015 lilikuwa ni kuboresha takwimu za Pato la Taifa ili ziweze kuakisi vyema shughuli za kiuchumi katika Nchi. Vile vile, kuhakikisha upatikanaji wa takwimu linganifu kimataifa kwa mujibu wa Mfumo wa Mwaka 2008.

## 1.2 Umuhimu wa Marekebisho ya Pato la Taifa

Marekebisho ya takwimu za Pato la Taifa ni mchakato unaohusisha kubadilisha mwaka wa kizio uliopitwa na wakati na kutumia mwaka wa kizio wenye taarifa za hivi karibuni. Mwaka wa kizio ni mwaka wa rejea unaotumika kukokotoa takwimu linganifu za Pato la Taifa za miaka mbalimbali. Marekebisho ya takwimu za Pato la Taifa yanafanyika kwa sababu zifuatazo:

i. Takwimu za mwaka wa kizio 2007 zimepitwa na wakati hivyo kushindwa kutoa taswira halisi ya mabadiliko ya muundo wa uchumi kwa wakati huo;

ii. Kujumuisha mabadiliko yaliyojitokeza katika uchumi kwenye mfumo wa uzalishaji bidhaa, matumizi na uwekezaji;

iii. Kuhuisha mabadiliko ya bei za bidhaa mbali mbali yaliyotokea katika kipindi hicho;

iv. Kuhuisha orodha ya bidhaa mpya zinazokuwa zimeingia kwenye uchumi kutokana na kukua kwa tekonolojia na kuondosha bidhaa ambazo hazipo sokoni;

v. Kujumuisha taarifa zote mpya kutoka katika taarifa za kiutawala, sensa na tafiti zilizofanyika miaka ya karibuni; na

vi. Kuzingatia matakwa mapya ya Mfumo wa Kimataifa wa Kutayarisha takwimu za Pato la Taifa na miongozo ya kuainisha shughuli za kiuchumi.

## 1.3 Vyanzo vya Taarifa za Marekebisho ya Takwimu za Pato la Taifa

Shughuli zote za kiuchumi zinazofanyika nchini zilijumuishwa wakati wa kufanya marekebisho ya takwimu za Pato la Taifa. Vyanzo vya taarifa zilizotumika kukokotoa takwimu za Pato la Taifa ni Sensa, Tafiti mbalimbali, taarifa za kiutawala na tafiti maalum zenye lengo la kujazia takwimu pale ambapo vyanzo vingine havikuweza kutoa taarifa za kutosheleza.

Taarifa zilizotumika katika kuandaa takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka wa kizio 2015 Tanzania Bara ni pamoja na:

- Sensa na Tafiti mbalimbali: Utafiti wa Matumizi na Mapato wa Kaya Binafsi 2011/12, Tafiti ya Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi 2014, Sensa ya Kilimo 2007/08, Utafiti wa Kilimo 2014/15, Sensa ya Uzalishaji Viwandani 2013 na Utafiti wa Mwaka wa Uzalishaji Viwandani 2015;
- Vyanzo vingine: Taarifa za kiutawala za uagizaji na uuzaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi, takwimu za mapato na matumizi ya serikali pamoja na takwimu za kodi ya ongezeko la thamani; na
- Tafiti maalum: Utafiti wa Shughuli za Biashara *(Trade Margin Study 2015)* na Utafiti wa Asasi zisizo za kiserikali zinazohudumia Kaya Binafsi *(Non-Profit Institutions Servings Households 2015).*

### 1.4 Mbinu Zilizotumika Kutayarisha Pato la Taifa kwa Mwaka Kizio 2015

Maboresho ya Takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka wa kizio 2015 zilitumia mbinu ya Mizania ya Ugavi na Matumizi (***Supply and Use Tables)*** ambayo inawezesha kupatikana kwa takwimu za Pato la Taifa kwa njia za Uzalishaji wa Bidhaa na Huduma *(Production Approach),* Matumizi *(Expenditure Approach)* na Mapato *(Income Approach).*

### 1.5 Upatikanaji wa Takwimu za Pato la Taifa Zilizorekebishwa

Muhtasari huu ni sehemu ya Taarifa ya kina ya Takwimu za Pato la Taifa kwa mwaka wa kizio 2015 Tanzania Bara ijulikanayo kama Vyanzo na Mbinu za Ukokotoaji wa Takwimu za Pato la Taifa 2019 inayopatikana katika Maktaba ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu Makao Makuu iliyopo Jengo la Takwimu Barabara ya Jakaya Kikwete, Dodoma pia kupitia tovuti www.nbs.go.tz au www.tanzania.go.tz.

## 2.0 TAKWIMU ZA PATO LA TAIFA ZILIZOREKEBISHWA

Marekebisho ya Takwimu za Pato la Taifa mwaka wa kizio 2015 yalizingatia miongozo, kanuni, mbinu na mifumo inayokubalika Kimataifa. Maboresho yaliyofanyika ni pamoja na:

i. Vyanzo vya Taarifa: Marekebisho ya takwimu za Pato la Taifa yametumia taarifa za hivi karibuni kutoka vyanzo vipya kama vile Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya 2011/2012, Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi 2014, Sensa ya Kilimo 2007/08, Utafiti wa Asasi zisizo za kiserikali zinazohudumia Kaya Binafsi 2015, Sensa ya Uzalishaji Viwandani 2013, Utafiti wa Mwaka wa Uzalishaji Viwandani, Utafiti wa Kufuatilia Kaya *(National Panel Survey*) 2014, Utafiti Maalum wa Shughuli za Biashara

*(Trade Margin)* 2015, Utafiti wa Ajira na Mapato *(Employment and Earnings Survey*) 2015 na taarifa za Kiutawala;

ii. Mbinu: Ukokotoaji wa Pato la Taifa kwa mwaka wa kizio 2015 ulitumia mfumo wa Mizania ya Ugavi na Matumizi *(Supply and Use Table).* Ongezeko la thamani kwa kila shughuli ya kiuchumi linapatikana kwa kutafuta tofauti ya zao ghafi na gharama za kati (*intermediate consumption*). Ukokotoaji wa ongezeko la thamani linalohusu shughuli za Serikali kwa upande wa Utawala na Ulinzi, Elimu na Afya umetumia gharama za Serikali zilizotumika katika uendeshaji wa shughuli hizo. Pia taarifa ya Ushuru wa Mabenki ***(FISIM)*** umegawanywa katika shughuli zote za kiuchumi;

iii. Wigo wa Shughuli za Kiuchumi*:* Pato la Taifa kwa mwaka wa kizio 2015 limejumuisha baadhi ya pato ghafi la shughuli za kiuchumi ambazo siyo rasmi *(Informal Sector Activities);* na

iv. Matakwa ya Kimataifa: Uandaji wa takwimu za Pato la Taifa umezingatia Mfumo wa Kimataifa wa Mwaka 2008 na Mwongozo wa kuanisha shughuli mbali mbali za kiuchumi unaojulikana kama *International Standard Industrial Classification of all economic activities Revision 4* (ISIC Rev. 4).

## 3.0 MATUMIZI YA TAKWIMU ZA PATO LA TAIFA

Takwimu za Pato la Taifa huandaliwa kwa lengo la kupanga mipango ya Serikali, Sekta Binafsi na Jamii yote kwa ujumla. Matumizi makubwa ya takwimu hizo ni kama ifuatavyo:

i. Kutathmini hali ya ukuaji wa uchumi wa Nchi katika kipindi husika;
ii. Kupanga mipango ya maendeleo na kutoa maamuzi;
iii. Kupima mchango wa shughuli mbalimbali za kiuchumi na ukuaji wake katika kipindi husika;
iv. Ni msingi wa utayarishaji wa bajeti ya Serikali;
v. Kulinganisha uchumi wa nchi na nchi nyingine duniani;
vi. Kuthathimini mabadiliko yanayotokea katika uchumi;
vii. Ni kigezo cha ujazi wa fedha nchini; na
viii. Ni kigezo kimojawapo kinachotumiwa na nchi wakati wa kukopa;


# 4.0 MUHTASARI WA MATOKEO YA MAREKEBISHO

## 4.1 Matokeo Muhimu

Taarifa hii inatoa muhtasari wa matokeo ya marekebisho ya takwimu za Pato la Taifa kwa kutumia kizio cha mwaka 2015. Aidha, matokeo haya yanatumika kufanya ulinganifu wa hali ya mabadiliko yaliyojionesha katika uchumi kwa kulinganisha mwaka wa kizio 2007. Pato la Taifa la mwaka 2015 kwa bei za miaka husika kwa kizio cha mwaka 2015 lilikuwa shilingi za Tanzania Trilioni 94.3 ikilinganishwa na Pato la Taifa la mwaka 2015 kwa bei za miaka husika kwa kizio cha mwaka 2007 lilikuwa shilingi za Tanzania Trilioni 90.8 **( Ang. Chati Na. 1**).

Kwa ujumla matokeo ya marekebisho ya mwaka wa kizio 2015 yanaonesha shughuli za Kilimo, Misitu na Uvuvi kupungua wakati shughuli za Viwanda na Ujenzi pamoja Huduma zikiongezeka ikilinganishwa na mwaka wa kizio 2007.


Chati Na. 1: Ongezeko la Thamani kwa Shughuli za Kiuchumi mwaka 2015 , kwa Kutumia Takwimu za Mwaka wa Kizio 2007 na 2015




## 4.2 Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa

Mwaka 2015, mchango wa shughuli za kiuchumi za Kilimo, Misitu na Uvuvi katika la Pato la Taifa ulipungua kufikia asilimia 26.7 kwa mwaka wa kizio 2015 ikilinganisha na asilimia 28.6 za mwaka wa kizio 2007. Hata hivyo, mchango wa shughuli za Viwanda na Ujenzi pamoja na Huduma ziliongezeka kwa asilimia 24.5 na 40.4 kwa mwaka wa kizio 2015 ukilinganisha na asilimia 24.0 na 39.5 kwa mwaka wa kizio 2007 kwa mfuatano huo ( **Ang. Chati 2**).

Chati Na. 2: Mchango katika Pato la Taifa kwa mwaka 2015; Mwaka wa Kizio 2007 na 2015




## 4.3 Viwango vya Ukuaji na Mchango wa Ukuaji katika Uchumi

Viwango vya ukuaji wa Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015 kuanzia mwaka 2013 na 2017 unaonesha kiwango cha juu kilikuwa asilimia 6.9 mwaka 2016 na kiwango cha chini kilikuwa asilimia 6.2 kwa mwaka 2015 (Ang. **Chati 3**). Aidha, ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2017 ulifikia asilimia 6.8, ukuaji huu ulichangiwa na shughuli za kiuchumi za Viwanda na Ujenzi kwa asilimia 40.3, zikifuatiwa na shughuli za Huduma kwa asilimia 31.3, shughuli za Kilimo, Msitu na Uvuvi kwa asilimia 23.0 na kodi ukiondoa ruzuku asilimia 5.4 ( **Ang. Jedwali 1**).

Chati 3: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015



**Jedwali Namba 1: Mchango wa Ukuaji wa Uchumi Mwaka 2017**

| Shughuli za kiuchumi | Mwaka wa kizio 2015 |
|---|---|
| Kilimo, Misitu na Uvuvi | 23.0 |
| Viwanda na Ujenzi | 40.3 |
| Huduma | 31.3 |
| Kodi toa ruzuku | 5.4 |

## 4.4 Pato la Wastani la Mwananchi

Pato la Wastani la Mwananchi kwa mwaka hupima kiasi ambacho kila Mwanachi atapata endapo Pato la Taifa lingegawanywa kwa usawa kwa kila Mwananchi. Pato la Wastani la Mwananchi hukokotolewa kwa kugawanya Pato la Taifa kwa idadi ya watu waliopo kwa mwaka husika. Pato la wastani la Mwananchi kwa takwimu zilizorekebishwa kwa kizio cha mwaka 2015, linaonesha kuongezeka kutoka shilingi za Tanzania 1,621,445 mwaka 2013 hadi shilingi za Tanzania 2,329,347 mwaka 2017 (Jedwali 2).

**Jedwali Na. 2: Pato la wastani la Mwananchi kwa mwaka wa Kizio 2015 katika Shilingi za Tanzania**

| | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 |
|---|---|---|---|---|---|
| Pato la Wastani la Mwananchi Kizio cha 2015 - Shs. | 1,621,445 | 1,778,840 | 1,968,965 | 2,191,190 | 2,329,347 |

## 4.5 Viwango vya Ukuaji, Takwimu za Pato la Taifa kwa Robo Mwaka


Takwimu za Pato la Taifa kwa Robo Mwaka hutumika kutathmini shughuli za kiuchumi za uzalishaji wa bidhaa na huduma katika vipindi vifupi vya miezi mitatu. Vipindi vya robo mwaka vinafuata mwaka wa kalenda ambapo vipindi hivyo ni Robo ya Kwanza (Januari - Machi), Robo ya Pili (Aprili - Juni), Robo ya Tatu (Julai - Septemba) na Robo ya Nne (Oktoba - Desemba).

Takwimu za Pato la Taifa kwa Robo Mwaka zilizotangulia hutofautiana na takwimu kama hizo zinazofuata kutokana na utaratibu unaokubalika kimataifa wa kurekebisha takwimu za Pato la Taifa kila baada ya miaka mitano au kutokana na kusuluhisha takwimu za vipindi vifupi vya robo mwaka zinazotumika kubaini mabadiliko katika uchumi katika kipindi hicho na zile za mwaka mzima ambazo ni za kina na zina taarifa sahihi.

Mwaka 2018, takwimu za Pato la Taifa kwa Robo mwaka zilizorekebishwa kizio cha 2015 zinaonesha kasi ya ukuaji ya asilimia 7.1 ilikuwa katika Robo ya Kwanza (Januari hadi Machi 2018) wakati kasi ya asilimia 6.3 ilikuwa katika Robo ya Pili yam waka (Aprili hadi Juni 2018). Katika Robo ya Tatu ya Mwaka (Julai hadi Septemba 2018) kasi ya ukuaji ilikuwa asilimia 6.8.

**Kwa msingi huo, wastani wa kasi ya ukuaji katika kipindi cha Januari hadi Septemba, 2018 ilikuwa asilimia 6.7.** Kasi ya ukuaji katika robo ya Nne mwaka 2018 itapatikana katika Taarifa ya Pato la Taifa kwa Robo Mwaka inayotarajiwa kutolewa mwishoni mwa mwezi Machi, 2019.

Chati Na. 4: Ukuaji wa Pato la Taifa Kwa Robo Mwaka, Mwaka wa Kizio 2015




## 6.0 VIAMBATISHI


Kiambatishi 1: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi Mwaka 2015 Mwaka wa kizio 2007 na 2015 .......... 10
Asilimia .......... 10
kiambatishi 2: Pato la Taifa (GDP) kwa Shughuli za Kiuchumi, Bei za Miaka inayohusika .......... 11
Asilimia .......... 12
Kiambatisho 4: Pato La Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi, Bei za Soko za Mwaka 2015 .......... 13
Kiambatishi 5: Ukuaji Halisi wa Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi, Kwa bei za mwaka 2015 .......... 14
Asilimia .......... 14
Shilingi Bilioni .......... 15
kiambatishi 7: Pao la Taifa na Matumizi yake, Bei za Miaka Husika .......... 15
Kiambatishi 8: Ukuzaji Rasilimali kwa Aina ya Shughuli, Bei za Mwaka 2015 .......... 15
Kiambatishi 9: Ukuzaji Rasilimali kwa Aina ya Shughuli, Bei za Miaka Husika .......... 16

**Kiambatishi 1: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi Mwaka 2015 Mwaka wa kizio 2007 na 2015**

**Asilimia**

| **Shughuli za Kiuchumi** | **MCHANGO WA PATO LA TAIFA 2015** | |
|---|---|---|
| | **MWAKA WA KIZIO 2007** (%) | **MWAKA WA KIZIO 2015** (%) |
| **Kilimo, Misitu na uvuvi** | **26.8** | **26.7** |
| Mazao | 13.5 | **14.1** |
| Mifugo | 9.4 | **7.6** |
| Misitu | 2.4 | **3.1** |
| Uvuvi | 1.6 | **2.0** |
| **Viwanda na Ujenzi** | **20.2** | **24.5** |
| Uchimbaji madini na mawe | 3.5 | **4.3** |
| Viwanda | 7 | **7.9** |
| Umeme | 0.9 | 0.8 |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 0.9 | 0.4 |
| Ujenzi | 7.9 | 11.1 |
| **Huduma** | **47.4** | **40.4** |
| Biashara na Matengenezo | 9.9 | 9.3 |
| Usafirishaji na uhifadhi mizigo | 5.9 | 7.3 |
| Malazi na Huduma za vyakula | 1.8 | 1.5 |
| Habari na Mawasiliano | 2.3 | 1.8 |
| Shughuli za Fedha na Bima | 2.8 | 4.4 |
| Upangishaji Nyumba | 6 | 3.1 |
| Shughuli za Kitaalamu, Kisayansi na Kiufundi | 1.2 | 0.5 |
| Shughuli nyingine za kiutawala na Huduma | 3.0 | 2.3 |
| Utawala na Ulinzi | 8.1 | 4.8 |
| Elimu | 3.2 | 2.6 |
| Afya na Ustawi wa Jamii | 1.6 | 1.5 |
| *Sanaa na Burudani* | *0.3* | 0.3 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 1.0 | 0.8 |
| Shughuli za Kaya Binafsi katika kuajiri | 0.3 | 0.2 |
| Toa Ushuru wa Huduma za Mabenki | -1.2 | 0.0 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **93.2** | **91.7** |
| Ongeza Kodi katika Bidhaa | 6.8 | 8.3 |
| **GDP at market prices** | **100** | **100** |

**Kiambatishi 2: Pato la Taifa (GDP) kwa Shughuli za Kiuchumi, Bei za Miaka inayohusika**

Shilingi Bilioni

| Shughuli za Kiuchumi | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Kilimo, Misitu na uvuvi*** | ***16,546*** | ***19,551*** | ***21,314*** | ***25,235*** | ***29,739*** | ***34,158*** |
| Mazao | 8,797 | 10,501 | 11,562 | 13,279 | 16,475 | 19,707 |
| Mifugo | 4,633 | 5,579 | 5,585 | 7,158 | 8,205 | 8,858 |
| Misitu | 1,737 | 2,069 | 2,478 | 2,920 | 3,095 | 3,310 |
| Uvuvi | 1,353 | 1,376 | 1,659 | 1,843 | 1,930 | 2,246 |
| Huduma za katika shughuli za Kilimo | 25 | 26 | 30 | 33 | 35 | 38 |
| ***Viwanda na Ujenzi*** | ***15,829*** | ***18,570*** | ***20,768*** | ***23,104*** | ***26,937*** | ***29,829*** |
| Uchimbaji madini na mawe | 3,072 | 3,125 | 3,098 | 4,056 | 5,299 | 5,206 |
| Viwanda | 5,882 | 6,649 | 7,534 | 7,412 | 8,467 | 9,102 |
| Umeme | 523 | 550 | 819 | 799 | 473 | 497 |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 279 | 324 | 372 | 391 | 433 | 530 |
| Ujenzi | 6,073 | 7,922 | 8,946 | 10,447 | 12,265 | 14,494 |
| ***Huduma*** | ***25,309*** | ***29,385*** | ***34,112*** | ***38,147*** | ***42,747*** | ***45,069*** |
| Biashara na Matengenezo | 6,448 | 7,064 | 8,046 | 8,748 | 9,862 | 10,843 |
| Usafirishaji na uhifadhi mizigo | 3,748 | 5,246 | 6,167 | 6,930 | 7,549 | 7,898 |
| Malazi na Huduma za vyakula | 1,254 | 1,317 | 1,330 | 1,422 | 1,523 | 1,605 |
| Habari na Mawasiliano | 1,282 | 1,433 | 1,599 | 1,681 | 1,740 | 1,829 |
| Shughuli za Fedha na Bima | 2,562 | 2,541 | 3,615 | 4,189 | 5,269 | 4,790 |
| Upangishaji Nyumba | 2,308 | 2,551 | 2,721 | 2,950 | 3,162 | 3,334 |
| Shughuli za Kitaalamu, Kisayansi na Kiufundi | 283 | 353 | 434 | 518 | 618 | 727 |
| Shughuli nyingine za kiutawala na Huduma | 1,243 | 1,523 | 1,914 | 2,184 | 2,662 | 3,027 |
| Utawala na Ulinzi | 2,882 | 3,615 | 3,974 | 4,549 | 4,846 | 4,986 |
| Elimu | 1,499 | 1,728 | 2,027 | 2,413 | 2,673 | 2,864 |
| Afya na Ustawi wa Jamii | 1,011 | 1,114 | 1,233 | 1,419 | 1,540 | 1,681 |
| Sanaa na Burudani | 174 | 195 | 223 | 249 | 286 | 322 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 474 | 556 | 662 | 718 | 831 | 959 |
| Shughuli za Kaya Binafsi katika kuajiri | 139 | 148 | 166 | 178 | 186 | 202 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **57,683** | **67,506** | **76,193** | **86,485** | **99,424** | **109,056** |
| Ongeza Kodi katika Bidhaa | 4,635 | 5,471 | 6,410 | 7,865 | 8,939 | 9,788 |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **62,319** | **72,977** | **82,603** | **94,349** | **108,362** | **118,844** |

**Kiambatisho 3: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato La Taifa, Bei za Miaka inayohusika**

Asilimia

| Shughuli za Kiuchumi | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Kilimo, Misitu na uvuvi*** | ***26.6*** | ***26.8*** | ***25.8*** | ***26.7*** | ***27.4*** | ***28.7*** |
| Mazao | 14.12 | 14.39 | 14.00 | 14.07 | 15.20 | 16.58 |
| Mifugo | 7.43 | 7.65 | 6.76 | 7.59 | 7.57 | 7.45 |
| Misitu | 2.79 | 2.84 | 3.00 | 3.10 | 2.86 | 2.79 |
| Uvuvi | 2.17 | 1.89 | 2.01 | 1.95 | 1.78 | 1.89 |
| Huduma za katika shughuli za Kilimo | 0.04 | 0.04 | 0.04 | 0.03 | 0.03 | 0.03 |
| **Viwanda na Ujenzi** | ***25.40*** | ***25.45*** | ***25.14*** | ***24.49*** | ***24.86*** | ***25.10*** |
| Uchimbaji madini na mawe | 4.93 | 4.28 | 3.75 | 4.30 | 4.89 | 4.38 |
| Viwanda | 9.44 | 9.11 | 9.12 | 7.86 | 7.81 | 7.66 |
| Umeme | 0.84 | 0.75 | 0.99 | 0.85 | 0.44 | 0.42 |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 0.45 | 0.44 | 0.45 | 0.41 | 0.40 | 0.45 |
| Ujenzi | 9.75 | 10.85 | 10.83 | 11.07 | 11.32 | 12.20 |
| **Huduma** | ***40.61*** | ***40.27*** | ***41.30*** | ***40.43*** | ***39.45*** | ***37.92*** |
| Biashara na Matengenezo | 10.35 | 9.68 | 9.74 | 9.27 | 9.10 | 9.12 |
| Usafirishaji na uhifadhi mizigo | 6.01 | 7.19 | 7.47 | 7.34 | 6.97 | 6.65 |
| Malazi na Huduma za vyakula | 2.01 | 1.80 | 1.61 | 1.51 | 1.41 | 1.35 |
| Habari na Mawasiliano | 2.06 | 1.96 | 1.94 | 1.78 | 1.61 | 1.54 |
| Shughuli za Fedha na Bima | 4.11 | 3.48 | 4.38 | 4.44 | 4.86 | 4.03 |
| Upangishaji Nyumba | 3.70 | 3.50 | 3.29 | 3.13 | 2.92 | 2.81 |
| Shughuli za Kitaalamu, Kisayansi na Kiufundi | 0.45 | 0.48 | 0.53 | 0.55 | 0.57 | 0.61 |
| Shughuli nyingine za kiutawala na Huduma | 2.00 | 2.09 | 2.32 | 2.31 | 2.46 | 2.55 |
| Utawala na Ulinzi | 4.62 | 4.95 | 4.81 | 4.82 | 4.47 | 4.20 |
| Elimu | 2.41 | 2.37 | 2.45 | 2.56 | 2.47 | 2.41 |
| Afya na Ustawi wa Jamii | 1.62 | 1.53 | 1.49 | 1.50 | 1.42 | 1.41 |
| Sanaa na Burudani | 0.28 | 0.27 | 0.27 | 0.26 | 0.26 | 0.27 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 0.76 | 0.76 | 0.80 | 0.76 | 0.77 | 0.81 |
| Shughuli za Kaya Binafsi katika kuajiri | 0.22 | 0.20 | 0.20 | 0.19 | 0.17 | 0.17 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **92.56** | **92.50** | **92.24** | **91.66** | **91.75** | **91.76** |
| Ongeza Kodi katika Bidhaa | 7.44 | 7.50 | 7.76 | 8.34 | 8.25 | 8.24 |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** | **100.0** |

**Kiambatisho 4: Pato La Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi, Bei za Soko za Mwaka 2015**

**Shilingi Bilioni**

| Shughuli za Kiuchumi | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| ***Kilimo, Misitu na uvuvi*** | ***21,807*** | ***22,408*** | ***23,952*** | ***25,235*** | ***26,436*** | ***28,012*** |
| Mazao | 10,807 | 11,283 | 12,344 | 13,279 | 13,996 | 14,899 |
| Mifugo | 6,205 | 6,503 | 6,821 | 7,158 | 7,507 | 7,877 |
| Misitu | 2,579 | 2,696 | 2,825 | 2,920 | 3,035 | 3,180 |
| Uvuvi | 2,188 | 1,896 | 1,930 | 1,843 | 1,865 | 2,020 |
| Huduma za katika shughuli za Kilimo | 29 | 30 | 31 | 33 | 34 | 36 |
| **Viwanda na Ujenzi** | ***17,987*** | ***19,872*** | ***21,057*** | ***23,104*** | ***25,818*** | ***28,574*** |
| Uchimbaji madini na mawe | 3,315 | 3,465 | 3,687 | 4,056 | 4,357 | 4,589 |
| Viwanda | 6,067 | 6,293 | 6,920 | 7,412 | 8,213 | 8,890 |
| Umeme | 669 | 724 | 815 | 799 | 869 | 878 |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 358 | 368 | 382 | 391 | 418 | 453 |
| Ujenzi | 7,578 | 9,023 | 9,253 | 10,447 | 11,961 | 13,765 |
| **Huduma** | ***31,224*** | ***32,809*** | ***35,864*** | ***38,147*** | ***40,550*** | ***42,691*** |
| Biashara na Matengenezo | 7,371 | 7,682 | 8,444 | 8,748 | 9,261 | 9,821 |
| Usafirishaji na uhifadhi mizigo | 5,710 | 6,051 | 6,578 | 6,930 | 7,325 | 7,816 |
| Malazi na Huduma za vyakula | 1,344 | 1,356 | 1,398 | 1,422 | 1,480 | 1,528 |
| Habari na Mawasiliano | 1,267 | 1,414 | 1,560 | 1,681 | 1,719 | 1,824 |
| Shughuli za Fedha na Bima | 3,444 | 3,406 | 3,764 | 4,189 | 4,236 | 4,115 |
| Upangishaji Nyumba | 2,606 | 2,715 | 2,829 | 2,950 | 3,077 | 3,212 |
| Shughuli za Kitaalamu, Kisayansi na Kiufundi | 322 | 385 | 448 | 518 | 606 | 694 |
| Shughuli nyingine za kiutawala na Huduma | 1,417 | 1,661 | 1,976 | 2,184 | 2,611 | 2,892 |
| Utawala na Ulinzi | 3,623 | 3,974 | 4,242 | 4,549 | 4,794 | 4,907 |
| Elimu | 1,923 | 1,928 | 2,186 | 2,413 | 2,665 | 2,859 |
| Afya na Ustawi wa Jamii | 1,285 | 1,245 | 1,350 | 1,419 | 1,498 | 1,612 |
| Sanaa na Burudani | 198 | 213 | 231 | 249 | 280 | 308 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 550 | 612 | 685 | 718 | 815 | 912 |
| Shughuli za Kaya Binafsi katika kuajiri | 162 | 167 | 172 | 178 | 183 | 189 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **71,018** | **75,089** | **80,873** | **86,485** | **92,804** | **99,278** |
| Ongeza Kodi katika Bidhaa | 6,962 | 8,179 | 8,001 | 7,865 | 8,025 | 8,393 |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **77,980** | **83,268** | **88,874** | **94,349** | **100,828** | **107,670** |

**Kiambatishi 5: Ukuaji Halisi wa Pato la Taifa kwa shughuli za kiuchumi, Kwa bei za mwaka 2015**

Asilimia

| **Shughuli za Kiuchumi** | **2013** | **2014** | **2015** | **2016** | **2017** |
|---|---|---|---|---|---|
| ***Kilimo, Misitu na uvuvi*** | ***2.8*** | ***6.9*** | ***5.4*** | ***4.8*** | ***6*** |
| Mazao | 4.4 | 9.4 | 7.6 | 5.4 | 6.4 |
| Mifugo | 4.8 | 4.9 | 4.9 | 4.9 | 4.9 |
| Misitu | 4.5 | 4.8 | 3.4 | 3.9 | 4.8 |
| Uvuvi | -13.3 | 1.8 | -4.5 | 1.2 | 8.3 |
| Huduma za katika shughuli za Kilimo | 2.5 | 6.1 | 4.5 | 4 | 5.5 |
| **Viwanda na Ujenzi** | ***10.5*** | ***6*** | ***9.7*** | ***11.7*** | ***10.7*** |
| Uchimbaji madini na mawe | 4.5 | 6.4 | 10 | 7.4 | 5.3 |
| Viwanda | 3.7 | 10 | 7.1 | 10.8 | 8.2 |
| Umeme | 8.2 | 12.7 | -2 | 8.8 | 1 |
| Usambazaji maji safi na udhibiti maji taka | 2.7 | 3.8 | 2.4 | 6.9 | 8.5 |
| Ujenzi | 19.1 | 2.5 | 12.9 | 14.5 | 15.1 |
| **Huduma** | ***5.1*** | ***9.3*** | ***6.4*** | ***6.3*** | ***5.3*** |
| Biashara na Matengenezo | 4.2 | 9.9 | 3.6 | 5.9 | 6.1 |
| Usafirishaji na uhifadhi mizigo | 6 | 8.7 | 5.4 | 5.7 | 6.7 |
| Malazi na Huduma za vyakula | 0.9 | 3.1 | 1.7 | 4.1 | 3.2 |
| Habari na Mawasiliano | 11.6 | 10.3 | 7.8 | 2.2 | 6.2 |
| Shughuli za Fedha na Bima | -1.1 | 10.5 | 11.3 | 1.1 | -2.8 |
| Upangishaji Nyumba | 4.2 | 4.2 | 4.3 | 4.3 | 4.4 |
| Shughuli za Kitaalamu, Kisayansi na Kiufundi | 19.5 | 16.3 | 15.7 | 17 | 14.5 |
| Shughuli nyingine za kiutawala na Huduma | 17.2 | 19 | 10.5 | 19.6 | 10.8 |
| Utawala na Ulinzi | 9.7 | 6.7 | 7.2 | 5.4 | 2.4 |
| Elimu | 0.3 | 13.4 | 10.4 | 10.4 | 7.3 |
| Afya na Ustawi wa Jamii | -3.1 | 8.4 | 5.1 | 5.6 | 7.6 |
| Sanaa na Burudani | 7.1 | 8.5 | 7.7 | 12.7 | 9.9 |
| Huduma nyingine za Kijamii | 11.3 | 12 | 4.7 | 13.5 | 12 |
| Shughuli za Kaya Binafsi katika kuajiri | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 3.2 |
| **Jumla ya Ongezeko la Thamani** | **5.7** | **7.7** | **6.9** | **7.3** | **7** |
| Ongeza Kodi katika Bidhaa | 17.5 | -2.2 | -1.7 | 2 | 4.6 |
| **Jumla ya Pato la Taifa (GDPmp)** | **6.8** | **6.7** | **6.2** | **6.9** | **6.8** |

Kiambatisho 6: Pato la Taifa na Matumizi yake Kwa Bei za mwaka 2015

**Shilingi Bilioni**

| Aina ya Matumizi | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2,017 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Matumizi ya mwisho (Final consumption)** | 59,307 | 61,882 | 65,251 | 69,620 | 70,595 | 73,614 |
| Serikali | 7,770 | 8,059 | 8,548 | 9,366 | 9,667 | 9,772 |
| Binafsi | 51,371 | 53,642 | 56,501 | 60,047 | 60,698 | 63,589 |
| Taasisi binafsi Zinazotoa huduma za Kijamii | 166 | 181 | 201 | 206 | 230 | 253 |
| **Ukuzaji rasilimali** | 23,425 | 29,019 | 31,804 | 30,908 | 33,795 | 38,338 |
| Rasilimali ya kudumu | 22,298 | 26,190 | 28,082 | 30,070 | 34,878 | 40,377 |
| Mabadiliko ya Thamani (Changes in valuables) | 770 | 776 | 821 | 903 | 902 | 859 |
| Ongezeko la limbikizo | 356 | 2,053 | 2,901 | -66 | -1,986 | -2,897 |
| Mauzo nje | 15,183 | 14,675 | 15,924 | 16,138 | 16,138 | 15,481 |
| Bidhaa - fob | 9,657 | 8,407 | 8,815 | 8,709 | 8,061 | 7,806 |
| Huduma | 5,526 | 6,268 | 7,108 | 7,430 | 8,077 | 7,675 |
| Uagizaji | 20,548 | 22,796 | 23,546 | 22,316 | 20,331 | 18,879 |
| Bidhaa - fob | 15,864 | 17,946 | 18,355 | 16,955 | 15,631 | 15,311 |
| Huduma | 4,684 | 4,850 | 5,191 | 5,361 | 4,700 | 3,568 |
| Makosa na Mapungufu | 613 | 489 | -558 | 0 | 632 | -883 |
| **Pato la Taifa kwa Bei za Soko (GDPmp)** | **77,980** | **83,268** | **88,874** | **94,349** | **100,828** | **107,670** |

**kiambatishi 7: Pao la Taifa na Matumizi yake, Bei za Miaka Husika**

Shilingi Bilioni

| Aina ya Matumizi | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Matumizi ya mwisho (Final consumption)** | 48,841 | 56,171 | 62,298 | 69,620 | 74,762 | 81,593 |
| Serikali | 6,498 | 7,331 | 8,151 | 9,366 | 9,825 | 10,097 |
| Binafsi | 42,196 | 48,675 | 53,954 | 60,047 | 64,700 | 71,227 |
| Taasisi binafsi Zinazotoa huduma za Kijamii | 147 | 166 | 192 | 206 | 238 | 268 |
| **Ukuzaji rasilimali** | 21,715 | 27,345 | 31,103 | 30,908 | 34,865 | 40,427 |
| Rasilimali ya kudumu | 20,543 | 24,781 | 27,400 | 30,070 | 35,493 | 42,142 |
| Mabadiliko ya Thamani (Changes in valuables) | 806 | 767 | 756 | 903 | 1,105 | 1,006 |
| Ongezeko la limbikizo | 365 | 1,797 | 2,947 | -66 | -1,733 | -2,721 |
| Mauzo nje | 13,942 | 13,875 | 14,926 | 16,138 | 17,717 | 17,993 |
| Bidhaa - fob | 9,256 | 8,403 | 8,441 | 8,709 | 9,177 | 8,925 |
| Huduma | 4,686 | 5,471 | 6,484 | 7,430 | 8,540 | 9,069 |
| Uagizaji | 19,940 | 21,615 | 22,540 | 22,316 | 20,665 | 20,321 |
| Bidhaa - fob | 16,227 | 17,628 | 18,054 | 16,955 | 15,603 | 15,816 |
| Huduma | 3,713 | 3,986 | 4,486 | 5,361 | 5,063 | 4,504 |
| Makosa na Mapungufu | -2,239 | -2,799 | -3,184 | - | 1,683 | -849 |
| **Pato la Taifa kwa Bei za Soko (GDPmp)** | **62,319** | **72,977** | **82,603** | **94,349** | **108,362** | **118,844** |

**Kiambatishi 8: Ukuzaji Rasilimali kwa Aina ya Shughuli, Bei za Mwaka 2015**

Shilingi Bilioni

| Aina | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 14,856 | 19,218 | 19,485 | 22,808 | 27,513 | 32,837 |
| Vifaa vya Usafiri | 1,337 | 1,219 | 2,045 | 1,663 | 1,374 | 1,173 |
| Mitambo na Vifaa | 4,280 | 3,714 | 4,229 | 3,194 | 3,269 | 3,474 |
| Mitambo na Vifaa Vingine | 991 | 1,062 | 1,200 | 1,172 | 1,324 | 1,336 |
| Rasilimali za Mazao ya Mifug | 290 | 333 | 365 | 375 | 385 | 414 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Haki ya Umiliki, Utafiti na Maendeleo, Huduma za Kitalaam | 544 | 645 | 758 | 857 | 1,014 | 1,143 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **22,298** | **26,190** | **28,082** | **30,070** | **34,878** | 40,377 |

**Kiambatishi 9: Ukuzaji Rasilimali kwa Aina ya Shughuli, Bei za Miaka Husika**

Shilingi Bilioni

| Aina | 2012 | 2013 | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Majengo | 13,308 | 17,909 | 19,195 | 22,808 | 27,722 | 33,872 |
| Vifaa vya Usafiri | 1,429 | 1,395 | 1,829 | 1,663 | 1,515 | 1,414 |
| Mitambo na Vifaa | 4,199 | 3,599 | 4,154 | 3,194 | 3,430 | 3,757 |
| Mitambo na Vifaa Vingine | 876 | 988 | 1,157 | 1,172 | 1,367 | 1,441 |
| Rasilimali za Mazao ya Mifug | 254 | 298 | 331 | 375 | 425 | 462 |
| Haki ya Umiliki, Utafiti na Maendeleo, Huduma za Kitalaam | 478 | 592 | 734 | 857 | 1,034 | 1,197 |
| **Jumla ya Ukuzaji Rasilimali** | **20,543** | **24,781** | **27,400** | **30,070** | **35,493** | **42,142** |